

## Maswali

1. Mbona Daudi na Absalomu hawakupendana?
2. Absalomu alitaka kufanya nini?
3. Alifanya nini ili watu wampende?
4. Mbona alikuwa na mkutano wa siri?
5. Mbona Daudi aliogopa?
6. Mbona Absalomu alichagua Ahithofeli amusaidie?
7. Daudi alifanya nini kumpumbaza Absalomu?
8. Hushai alisaidiaje Daudi?
9. Absalomu alikufaje?
10. Mbona Mungu alimsaidia Daudi?

## Majibu

1. Kwa sababu hawakuelewana. Daudi alihuzunika kwa kuwa Absalomu aliuwa nduguye. Absalomu hakupenda njia aliyoitumia Daudi kwa kuamua shida.
2. Absalomu alitaka awe mfalme badala ya Daudi.
3. Absalomu alikaa karibu na lango la mji akiambia watu kwamba atakuwa muamuzi mzuri. Alichukuwa mikona yao akiwabusu, hiyo ilifanya watu wampende.
4. Absalomu alipanga kuwe na mkutano wa siri na wakuu wa serikali ili awashawishi wamchague awe mfalme.
5. Daudi aliogopa kwa sababu alijua Absalomu atamuua ili awe mfalme.
6. Absalomu alimchagua Ahithofeli kwa sababu alikuwa na busara alipomfanyia babake.
7. Daudi alimtumia Hushai ili ampumbaze Absalomu. Hushai alimpa Absalomu mashauri tofauti yasiyo ya kweli.
8. Hushai alimsaidia kwa kumwambia mpango aliompangia Absalomu.
9. Absalomu alikufa aliposhikwa nywele juu ya mtawi ya mti na Yoabu alipompata akamuua.
10. Mungu alimsaidia Daudi kwa sababu Daudi alimpenda na aliomba usaidizi wake.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



### Awamu ya 1 Mwaka wa 2

# 19 Daudi na Absalomu

## Marejeo

- 2 Samweli 15:1—14 & 32—37; 2 Samweli 17:14—16  
2 Samweli 18: 1—18

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu huwa na wale wampendao.

## Maneno maalum

1. Absalomu + Amnoni + ubishi + panda + Daudi + shida.
2. Absalomu + lango la mji + amua + miaka minne.
3. Mkutano wa siri + mfalme + Daudi + ogopa + toka Yerusalemu.
4. Ondoka + rafiki mwaminifu + chakula + Ahithofeli
5. Hushai anabusara + Ahithofeli + bubuaza Absalomu.
6. Hushai + mpango + Daudi + tayarisha majeshi
7. Efraimu + uwawa + nasa + Yoabu
8. Daudi ana wasiwasi + Absalomu alikufa + Mungu anazuia.

**19.1** Absalomu alikuwa mwana wa Daudi. Usiano wao haukuwa mzuri, siku moja Absalomu alibishana na ndugu yake Amnoni na akamua. Daudi alimpenda Absalomu sana lakini hakupenda vile aliamua mambo yake. Absalomu hakueelewa pia vile Daudi alishugulikia mambo yake. Alifikiri atakuwa mfalme mzuri kwa hivyo akaanza kutoa watu kwa baba yake.

**19.2** Alikuwa akikaa kwa lango la mji ili Mwisraeli yeyote aliyekuja na malalamishi kwa mfalme aliaamua na kuwambia, “Matakwa yenu ni ya haki. Kama mimi ningekuwa mwamuuzi ningemfanyia vile mnataka.” Angewashika mkono na kuwabusu kwa upendo. Alifanya hivyo kwa miaka minne na watu wakampenda kuliko mfalme Daudi.

**19.3** Ikawa siku moja akapanga mkutano wa siri. Akashawishi wafuasi wa Daudi na wakuu wa serikali kwamba yeye anaweza kuwa mfalme badala ya babake. Daudi aliposikia hayo, aliogopa. Aliamua kutoka Yerusalemu na kwenda mbali pahali pa usalama ili Absalomu asimpate.

**19.4** Kwa hivyo aliondoka na wafuasi wengine na marafiki wake waaminifu, wale waliompenda Mungu kwa kukumbuka kwamba Daudi alikuwa amechaguliwa na Mungu Walimsaidia kumletea maji na chakula. Wakati huo Absalomu alikuwa ameenda Yerusalemu kulikokuwa kiti cha enzi na jumba la mfalme. Alimchagua Ahithofeli kuwa mtu wa kumuelekeza kwa kila jambo. Ahithofeli alikuwa mfanya kazi wa Daudi lakini alimuasi. Sasa alifanyia Absalomu.

**19.5** Daudi alijua mashauri ya Ahithofeli yalikuwa ya busara. Akamtuma Hushai aende Yerusalemu na ajifanye rafiki kila

mara Ahithofeli akipeana mashauri, Hushai angeyapinga kumpumbaza na kumshauri tofauti. Huu mpango ulifaulu na mwishowe Absalomu alimsikiliza Hushai pekee.

**19.6** Hushai alimpangia Absalomu vile anaweza kushambulia watu wa Daudi na amkamate Daudi. Tena Hushai alitumia Daudi huo mpango kwa siri ili wajitayarisha wasishikwe wala wauwawe. Daudi alitayarisha jeshi lake na akaambia askari hivi, “Angalia sana msimuuwe mwanangu.”

**19.7** Siku ifwatayo majeshi ya Daudi na ya Absalomu walikutana kwa msitu wa Efraimu na wakapigana. Watu wa Daudi waliuwa watu wa Absalomu karibu wote. Wakati Absalomu alikuwa anatoroka kwa farasi wake nywele yake ilishikwa kwa mti. Farasi alitoroka akamuacha akining'inia juu. Mmoja wa wakuu wa jeshi la Daudi aitwaye Yoabu alipompata Absalomu, alikairi maagizo ya Daudi na akamua Absalomu.



**19.8** Daudi aliifurahi kwamba ameshinda vita, lakini alilia sana aliposikia mwanawe amekufa. Bahati mbaya Absalomu hakupenda Mungu na hakumhusisha awe naye. Kwa hivyo alishindwa kwa vita na akafa. Daudi alimpenda Mungu na Mungu akamlinda. Kwa hivyo alishinda kwa kusaidiwa na Mungu.